

HALMASHAURI YA WILAYA YA CHEMBA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W))

WILAYA YA CHEMBA
FAX/ SIMU: 026 2360175
BARUA PEPE: dedChemba@yahoo.com



S.L.P 830
CHEMBA.

04/04/ 2018

TANGAZO LA NAFASI KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba iliyopo katika Mkoa wa Dodoma, anapenda kuwatangazia watazania wote wenye sifa za kuajiriwa katika utumishi wa Umma kutuma maombi ya kazi. Hii ni kufuatia kibali cha ajira mbadala kwa Watendaji wa Vijiji/Mitaa chenye **Kumb Na.CFC. 26/205/01 "FF"/91** cha tarehe 22 Agosti, 2017 kikisomwa pamoja na barua ya nyongeza ya muda wa utekelezaji wa kibali cha ajira mbadala kwa Watendaji wa Vijiji/Mitaa yenye **Kumb Na. CFC.26.205/01"GG"/95** ya tarehe 12 Machi 2018 vilivyotolewa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

1.1 Mtendaji wa Kijiji Daraja III– Nafasi 33

Sifa za kuajiriwa :-

- Wahitimu wa kidato cha nne au sita waliohitimu mafunzo ya astashahada/cheti "Technician Certificate" katika moja ya fani zifuatazo; Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

MAJUKUMU

- a) Atakuwa Mtendaji Mkuu wa Kijiji na mshauri wa Serikali ya Kijiji na kamati zake katika Mipango ya Maendeleo.
- b) Kusimamia, kukusanya na kutunza kumbukumbu zote na Nyaraka za Kijiji.
- c) Atakuwa Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- d) Atakuwa kiongozi wa Wakuu wa Vitengo na Kitaalam katika Kijiji.
- e) Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala bora katika Kijiji
- f) Ataratibu na kusimamia utekelezaji wa sheria ndogondogo za Serikali ya kijiji.
- g) Atasimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji
- h) Atafanya kazi nyingine kama atakavyoelekezwa na mkuu wake wa kazi.
- i) Atakuwa Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.

Kiwango cha mshahara: TGS B – Tsh. 390,000/= kwa mwezi

MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI

- a) Barua ya maombi iandikwe kwa mkono kwa lugha ya Kiswahili au Kingereza.
- b) Picha 2 (mbili) ndogo za hivi hivi karibuni.
- c) Barua iambatanishwe na Wasifu binafsi wa mwombaji (CV) wa hivi karibuni.
- d) Barua ya maombi iambatanishwe na vivuli vya vyeti vya kuzaliwa, kidato cha nne, taaluma NTA5 kwa vyuo vilivyopo chini ya NACTE.
- e) Awe raia wa Tanzania ambaye ana umri chini ya miaka 45
- f) Asiwe amewahi kuhukumiwa kifungo jela au kufukuzwa kazi.
- g) Mwombaji awe tayari kufanya kazi Chemba pasipo kuhama ndani ya miaka mitatu.

- h) Matokeo ya muda (Provisional /Testimonial/Statement of Results) **HAVITAKUBALIWA.**
i) Waombaji wenye vyeti vya kidato cha nne na sita vya nje ya nchi vifanyiwe ulinganishi na NECTA na majibu yaambatishwe na barua ya maombi.

Mwisho wa kupokea maombi ni siku ya Jumatatu ya tarehe **20/04/2018 saa 09:30 Alasiri.**

Maombi yatumwe kwa **Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya ya Chemba, S.L.P 830, Chemba.**



DR. SEMISTATUS H. MASHIMBA
MKURUGENZI MTENDAJI (H/W)
CHEMBA

**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA YA
CHEMBA**

NB.Tangazo hili pia linapatikana kupitia Tovuti ya Halmashauri ambayo ni **www.chembadc.go.tz.**